



**TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA TANO (5) WA WANAHISA WA
SHIRIKA LA NDEGE LA PRECISION AIR**

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba, Mkutano Mkuu wa Tano (5) wa Wanahisa wa Shirika la Ndege la Precision Air utafanyika siku ya Ijumaa Tarehe 08 mwezi Novemba 2019 katika Ukumbi wa Mkutano wa Jengo la PSSSF Golden Jubilee Towers, Ghorofa ya 6, mtaa wa Ohio Dar es Salaam kuanzia saa Tatu kamili Asubuhi.

Ajenda ya Mkutano itakua kama ifuatavyo:

1. Kufungua Mkutano
2. Taarifa ya Mkutano na Akidi
3. Kupitisha Ajenda za Mkutano.
4. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano mkuu wa Nne wa Wanahisa uliofanyika tarehe 29 Agosti, 2016.
5. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Nne wa Wanahisa
6. Kupokea, kujadili na kupitisha Ripoti ya Wakurugenzi, Taarifa ya Mkaguzi wa Nje na Taarifa za Fedha zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi, 2018.
7. Uteuzi wa Wakurugenzi
8. Kupokea na kuidhinisha pendekezo la malipo ya Wakurugenzi.
9. Kupokea na kuidhinisha uteuzi wa Wakaguzi wa Nje wa Mahesabu kwa mwaka 2018/2019.
10. Mengineyo
11. Kufunga Mkutano.

Notisi hii imetolewa leo tarehe 17 Oktoba 2019

Mambo ya Kuzingatia:

1. Mwanahisa anayetarajia kuhudhuria Mkutano huu atatakiwa kufanya hivyo kwa gharama zake mwenyewe; na atatakiwa kufika na nakala yake ya Risiti ya Uwekezaji wa Hisa (Depository receipt), pamoja na kitambulisho chochote kati ya hizi:- Hati ya Kusafiria (Passport), Kitambulisho cha Taifa, Leseni ya Udereva au Kitambulisho cha Mpiga Kura.

2. Bodi ya Wakurugenzi imependekeza kwa Wanhisa kutolipwa kwa gawio kwa mwaka unaoisha tarehe 31 Machi, 2018.
3. Iwapo Mwanahisa anayeruhusiwa kuhudhuria Mkutano na kupiga kura, atashindwa kwa sababu zozote zile kuhudhuria Mkutano, ataruhusiwa kuchagua Mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata na kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni. Nakala ya fomu iliyosainiwa na Mwanahisa ifikishwe katika ofisi za Kampuni zilizopo Dar es Salaam kabla ya saa Tatu asubuhi (9am), Jumatano tarehe 06 Novemba, 2019.
4. Vitabu vyenye taarifa ya Mwaka pamoja na Fomu za Uwakilishi (Proxy Forms) zitapatikana katika tovuti ya Precision Air (<https://www.precisionairtz.com/about-us/investor-relations>) kuanzia Ijumaa tarehe 01 Novemba 2019. Nakala za Makabrasha ya Mkutano zitapatikana pia kwenye ofisi zetu za Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Moshi kuanzia Jumatano Tarehe 5 Novemba 2019.

KWA AGIZO LA BODI YA WAKURUGENZI

MIGIRE KEMBO MIGIRE

KATIBU WA KAMPUNI